# JARIDA LA KILIMO HIFADHI

**JUNI 2023 ● UJAZO NAMBA 9 ● NAKALA YA 2**


| **NDANI YA TOLEO HILI** | Kilimo Kama Biashara | Kusimulia Hadithi kwa Picha | Wasifu wa Mkulima wa Kilimo Hifadhi | Wasifu wa mshirika: Ofisi ya ODE (de Développement des Eglises Evangéliques) | RATIBA ZA SAFARI ZA ALTA |
|---|---|---|---|---|---|


## Kilimo Kama Biashara

***Lilian Zheke, Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha, Kusini mwa Africa***



**Kufikia usalama wa chakula kupitia uzalishaji wa chakula, kuachilia bidhaa kwa ajili ya kuuza.**

Kilimo biashara (FAAB) kinadumisha kilimo kama njia ya kuongeza faida. Kilimo biashara kinasaidia wakulima kubadili mawazo yao kutoka kwenye vitu Kwenda kwenye fikra ya kibiashara. Kama wakulima wataongeza uzalishaji kwa kutumia njia kama kilimo hifadhi plus, wana nafasi kubwa ya kuzalisha sio tu kwa matumizi lakini pia kuongeza kipato na mali zingine. Rasilimali za FAAB zinaweza zikapakuliwa hapa.

Biashara inafanya kazi kwa lengo la kupata faida kupitia kutoa huduma au bidhaa. Katika kilimo, vitendea kazi kama mbegu na shama vinatumika kuzalisha mazao au mifugo ambayo inauzwa kwenye masoko. Utendaji kazi wa biashara ya kilimo unaanza kwa kuuliza ni nini soko linahitaji. Kisha mkulima anapima faida zinazotokana na njia mbalimbali (biashara ndogondogo) na kupanga kuanza uzalishaji na shughuli za kutafuta masoko.Mwisho wa msimu, wakulima wanafanya tathmini kama malengo yao yametimizwa ili kuwasaidia kupanga kwa ajili ya msimu mwingine.

### KUWAJENGEA WAKULIMA UWEZO WA KIBIASHARA

Kwa wakulima kuendesha mashamba yao kibiashara, lazima wafanye maamuzi mazuri ya uzalishaji, masoko na kifedha ili kupunguza gharama,kupata masoko yenye faida, na kuongeza fkipato chao.Kwa nyongeza kufahamu namna ya kupanda mazao na kuongeza uzalishaji, wakulima wanahitaji uelewa na ujuzi wa kufanya maamuzi sahihi ambayo yataongeza faida kwao. Wakulima watahitaji:

- Kuchagua biashara sahihi (mazao na/mifugo);


Canadian Foodgrains Bank
A Christian Response to Hunger

**Washauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha wa Canadian Foodgrains Bank**

**John Mbae** john.mbae@tearfund.org
**Neil Rowe Miller** neil.rowe-miller@tearfund.org
**Jean Twilingiyumukiza** jean.twilingiyumukiza@tearfund.org
**Lilian Zheke** lilian.zheke@tearfund.org

- Tambua na kuweza kupata fursa za masoko;
- Fanya tathmini ya faida na changamoto;
- Andaa mpango wa biashara na bajeti;
- Endeleza rekodi nzuri na kusimamia fedha.

Masuala haya yana athari kubwa katika maendeleo na mafanikio ya biashara za kilimo.

## MPANGILIO WA KILIMO BIASHARA:

Mpangilio wa biashara unahusisha kuandaa na kupanga rasilimali zote zinazohitajika kuendesha biashara. Inaamua ni rasilimali gani zitahitajika, lini zitahitajika na wapi zitatokea. Mpango mzuri wa biashara ya kilimo utaelezea aina ya bidhaa itakayozaishwa, namna itakvyofanyika, rasilimali gani zitahitajika na lini, namna bidhaa itakavyouzwa na faida gani inatarajiwa.


Sylvia Muleya, KMTC bibi shamba kutoka Binga, Zimbabwe,akifanya zoezi la kuchagua biashara za kilimo.

## KUPANGA BAJETI NA KUKUZA FAIDA:

wakulima wanapaswa kufanya uchambuzi wa gharama watakazoingia na kuamua bei ili kuweza kupata faida. Uchambuzi wa faida ya jumla ni makadirio ya mapato, gharama na faida za kuzalisha bidhaa. Uchambuzi wa faida ya jumla unaweza kutumika kwa yafuatayo:

- Kadiria faida ya kiasi ya biashara ya mazao au mifugo tofauti;
- Linganisha uwezo wa faida katika nyakati tofauti katika mwaka;
- Amua namna ambavyo gharama zitapunguzwa ili kuongeza faida;
- Tambua uhitaji wa kuongeza bei au upatikanaji wa masoko yenye kulipa.

## MSINGI WA MASOKO:

mbinu za kuleta wateja ni muhimu sana katika biashara yeyote. Nyenzo za mafunzo ya wakulima kwa ajili ya mbinu za kuleta wateja zinaweza kupakuliwa kwenye kiungo hiki. Wakulima watahitaji kuchagua bidhaa nzuri, wanunuzi wazuri na muda mzuri wa kuzalisha na kuuza bidhaa zao. Ili kufanya haya wakulima watatakiwa kuweza:

- Kuelewa na kufanya utafiti wa mahitaji ya masoko na muelekeo (ikiwa ni Pamoja na ubora wa viwango, usambazaji na uhitaji na mabadiliko ya msimu);
- Kuandaa na kukutana na mahitaji ya soko;
- Kuanzisha mahusiano ya kibiashara ya kudumu kwa wanunuzi na watendaji wa masoko.

## UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU:

Biashara nzuri inatunza kumbukumbu ya kila kitu kinachohusika na biashara yao katika hali nzuri na kutunza taarifa hizo kwa ajili ya matumizi ya baadae.Wakulima wanapaswa kutunza kumbukumbu ya uzalishaji, matumizi, mapato mbinuu za kuleta wateja na nguvu kazi. Kumbukumbu hizi zitasaidia kufanya uchunguzi kama biashara

zao zinafaida mwaka hadi mwaka na kuanzisha mielekeo ya muda mrefu ambayo yanaweza kusaidia kuboresha faida zao kwa muda mrefu.

### UDHIBITI WA HALI HATARISHI:

Wakulima wanahitaji kuelewa hali hizi za hatari za biashara mbali mbali ili kuweza kuamua kama faida zitokanazo na biashara hizo zinazidi hali yoyote inayoonekana kuwa hatarishi, nak ama wakipata mbinu ya kudhibiti hali yoyote ya hatari na gharama za biashara ya kilimo. Kufanya uamuzi sahihi utahitaji kuwa na uelewa wa uwezekano wa hali hatarishi kutokea, athari zake kwenye biashara, mbinu dhabiti za kuzuia hali hiyo ya hatari,na gharama zitokanazo na mbinu hizo za kudhibiti.

### HITIMISHO:

sio wakulima wote wana utayari au uwezo wa kujitolea sehemu ya uzalishaji wao kwenda kwenye malengo ya biashara. Baadhi ya wakulima watahitaji kutatua masuala ya uzalishaji, ili kuweza kufikia usalama wa chakula, kabla ya kuzingatia mauzo. Mabadiliko kutoka kwenye kilimo kwa ajili ya chakula Kwenda kwenye uzalishaji wa kibishiara inachukua muda kwa wakulima wengi. Kuwasaidia, wafanyakazi wa miradi wanatakiwa kupata ujuzi na uelewa huu ili kuweza kuwasaidia wakulima kusogea kwenye kilimo kinachoendeshwa kibiashara na chenye tija.

---

## Kusimulia Hadithi kwa Picha

***Christina Philips, Mkurugenzi Rasilimali na Ushirikiano wa Umma***

Picha zinaweza kuonyesha taabu na njaa au zinaweza kuonyesha ushindi wa wakulima na jamii dhidi ya Ukosefu wa usalama wa chakula. Muongozo ufuatao unaonyesha namna gani picha zinaweza kutumika vizuri Kwa kuheshimu na kustahi adhama/heshima ya watu.

### NINI KINALETA PICHA KUWA SHIRIKISHI?



**Picha ya uzalishaji wa kilimo inaonyesha jamii inayojitegemea.**

### CHAKULA!

Usalama wa chakula upo katika kitovu cha kazi za na nk na inatakiwa ionekane katika picha. Picha zinazoonyesha uzalishaji wa kilimo, matumizi ya chakula na usambazaji ni muhimu katika simulizi zetu.



**Utayarishaji wa chakula na matumizi kuwasilisha uamuzi wa kibinafsi.**

## PICHA ZA MATUKIO!

Chukua picha ambayo inaonyesha wahusika wa mradi kama mashujaa wa simulizi zao ambao wanafanya kazi kwa bidii ili kuzalisha chakula na kulisha familia kuliko watazamaji. Picha zinazoonyesha shughuli mbalimbali, matumaini na harakati ndizo picha shirikishi.



**Picha za matukio zinatoa simulizi kamili.**

## KUJIANDAA NA TUKIO LA KUPIGA PICHA

- ***Pangilia muda wako!*** Pangilia muda zaidi ya ule unaofikiria kuwa utatumia kupiga picha na kuchukua video. Tegemea kuchukua muda kuwasaidia watu kukuamini kabla hata hujachukua picha. Upigaji picha mzuri unachukua muda mrefu kuliko uliotegemewa.
- ***Andaa orodha ya matukio unayoyataka.*** Panga kabla ya muda picha gani zitaelezea simulizi unayotaka kuitoa. Kumbuka kuzingatia picha zenye matukio! Tumia orodha ya matukio ikuongoze kwenye kipindi cha upigaji picha.
- ***Hakikisha uono wa kamera yako umewekwa juu kiasi cha kutosha!*** Uono wa kamera yako unaweka ukaitwa "ubora wa picha" au "ukubwa wa picha" na utaonyesha kiasi cha taarifa kilichonaswa kwenye picha. Uono ukiwa wa hali ya juu, ndipo picha itakapoonekana vizuri zaidi na bila giza/ukungu hasa ikikuzwa. Chagua kipimo chenye ukubwa zaidi ili kuhakikisha picha inanaswa vizuri. Kama ukubwa wa faili ni chini ya 1.0 MB, bai uonekanaji wa hiyo picha utakua hafifu. Kwa kuongeza (mfano: mabango au picha zitakazorushwa kwa projekta) ukubwa wa faili lazima uwe na ukubwa wa 5.0 MB au Zaidi.
- ***Sema lengo lako.*** Waeleze wahusika kwa nini unawapiga picha na zitatumikaje. Wajulishe kuwa picha zao zitaonekana kwenye machapisho mbalimbali na vyombo vya Habari kama vile vipeperushi, mitandao ya kijamii, magazeti n.k.
- ***Omba ridhaa yao:*** Watu wengine wanaweza kuwa tayari kutoa simulizi zao lakini sio picha kwa sababu za kiusalama. Heshimu uamuzi wao!! Pata kibali kwa maandishi, vinakili sauti au kwa video yeyote yenye kufaa kutumika.



**Hii picha ya shamba darasa la wakulima inaonyesha wanachama na familia zao Pamoja na namna wanavyojifunza kupanda mazao ya mafunika ardhi.**

## MUKTADHA!

Ukiangalia picha, unatakiwa kupata hisia ya simulizi. ukijumuisha na muktadha wa maisha ya mhusika inasaidia katika kupata hisia hii. Kwa mfano, kama ni wakulima, jumisha picha zao wakiwa wanafnya kazi shambani. Kama wako kwenye kikundi fulani, Piga picha zao wakiwa wanazungumza na wanakikundi wenzao katika vikundi vya kuhifadhi pesa, piga picha za wanakikundi wakiwa wanafanya kazi za kikundi.



**Katika picha hii tunaona hisia, na tunajifunza kuhusiana na familia ya mkulima kiongozi.**



**Mwanamke katika picha hii anaonekana kutokuwa na furaha,ila kama mtu mwenye maazimio Fulani.**

## HISIA!

Jaribu kuteka hisia.Ongea na watu wakati unawapiga picha. Mara nyingi watu wanafunguka wakati wa maongezi,na hapondipo unapaswa kupiga picha ambayo itateka hisia halisi. Katika picha zilizopo kulia, ni hisia gani unaziona?



**Lakini wanamke huyu,  anaonyesha furaha!**

## WAKATI WA KIPINDI CHA KUPIGA PICHA

- ***Chukua muda kuwafanya washiriki kujisikia huru.*** Jitambulishe na ueleze kwa nini unachukua picha. Kama utaonyesha hali ya kutokuwa huru,washiriki watajua. Kama utakuwa katika hali ya utulivu na kufurahia mazungumzo, ni wazi kwamba washiriki wako watakua katika hali ya utulivu pia.
- ***Chukua picha katika mpangilio tofauti na kuonyesha matukio tofauti tofauti.*** Hii inasaidia kutoa picha kamili ya simulizi ya mshiriki.
- ***Hakikisha kuwa picha hiyo itamuonyesha mshiriki kwa kujali utu wake.*** Haionyeshi hali yoyote mbaya ya ubaguzi, na hainyanyasi watu katika mazingira hatarishi.
- ***Wakati wa kuchukua picha za watoto, wahusishe wazazi ama walezi wake*** katika picha yenye mazingira ya watoto. CFGB inazuia matumizi ya picha za Watoto bila wazazi/walezi wao.
- ***Kusanya majinaa, umri na uhusiano wa watu katika picha zote.*** Weka kumbukumbu ya nani amepigapicha hiyo, jina la mradi na shirika linalo sapoti kazi zao.



**Picha za mlalo zinatumika mara nyingi kwenye mabango na uwasilishaji wa powerpoint.**

## PIGA PICHA ZA WIMA NA ZA MLALO.

Muelekeo unatumika kwa vifaa mbalimbali.  Geuza kamera yako ilikuhakikisha unapata mielekeo tofauti.



**Picha za wima mara nyingi zinatumika katika machapisho.**



Katika picha hii, mshiriki alikua akitazama upande wenye mwanga, na kufanya uso wake kuonekana vizuri.

## ACHA MWANGA UKUONGOZE UELEKEO WA KUPIGA PICHA YAKO.

Simama uelekeo ambao chanzo cha mwanga utakua nyuma yako ili kupunguza kivuli na kuhakikisha washiriki wako wanaonekana vizuri. Kama chanzo cha mwanga (mf. Jua) kitakua nyuma ya mshiriki wako wataonekana wako gizani na itakua vigumu kuona. Kama ni lazima upige picha kukiwa na mwanga nyuma ya mshiriki wako basi tafuta namna ambayo utaweka mmulika usoni ili aonekane vizuri kwenye picha



Mwanga uliopo nyuma ya watu katika picha hii inaleta ugumu katika kuona nyuso zao.

## WAKATI WAKUTUMA PICHA

- Kabla ya kutuma picha, jiulize maswali yafuatayo.
    1. Je watu waliopigwa picha watapends kuonekana hivi na kuchapishwa?
    2. Je picha hii haitaleta mtafaruku kwenye utamaduni wao? Kumbuka kuwa kinachoonekana kuwa chenye heshima inatofautiana kutoka tamaduni moja kwenda nyingine.
    3. Kwa namna gani picha hii itachukuliwa na watu wengine?
- ***Usitume picha ikiwa katika hali ya nakala.*** Microsoft Word inapunguza ubora wa picha ambapo inamaanisha kuwa haziwezi kutumika kwa ajili ya mawasiliano ya aina yoyote.
- ***Tuma picha tofauti kama kiambatanishi.*** Kama picha ni kubwa kuambatanisha, tumia dropbox, onedrive, google drive au huduma ya "WeTransfer." Wafanyakazi wa benki ya chakula na nafaka wanaweza kukusaidia kama haujui namna ya kufanya hivi.
- ***Husisha maelezo maupi kama sehemu ya simulizi yako, au kutenganisha waraka.*** Maelezo mafupi ya picha yanatakiwa kutoa taarifa/maelezo ambayo inaweza isiwe simulizi. Hii inaweza kuongeza thamani na kutafsiri picha za washiriki ambazo zinaweza kuwa na maana tofauti kwenye tamaduni zao.



Picha ya wima katika kona hii ya picha haionyeshi hali ya mwendo.

## TUMIA KONA TOFAUTI TOFAUTI.

Kwa kupiga picha katika kona tofauti, unaweza kunasa taarifa nyingi Zaidi, hisia au haiba ya mtu. Kama utapiga picha kwenye sehemu ambayo mandhari ya nyuma ambayo ni mbaya, badili muelekeo au panda sehemu ya juu alafu uangalie chini katika sehemu ya juu huwa inatoa muonekano wa tofauti.



Kwa sababu ya kona hii katika hii picha inaonyesha mtu yuko kwenye mwendo, inaifanya kuvutia Zaidi.

## Wasifu wa Mkulima wa Kilimo Hifadhi


Alemo Ayere in his CA maize-pigeon pea-cowpea field

Alemo Ayere alijifunza jinsi ya kutumia Kilimo Hifadhi kama mshiriki katika mradi wa usalama wa chakula wa Terapeza Development Association (TDA) nchini Ethiopia. Amekuwa akitumia kilimo hifadhi sasa kwa zaidi ya miaka 5, na anaelewa kwa uwazi manufaa ya kuboresha afya ya udongo na ongezeko la mavuno.

Licha ya kuelewa faida hizi, anatumia kilimo hifadhi kwenye sehemu ndogo tu ya shamba lake la hekta 4. Kizuizi kikuu kinachomzuia ni hitaji la nguvu kazi ya utayarishaji wa shamba na upandaji kwa mkono. Mnamo Mei, 2023, Ato Alemo iliandaa kipindi cha mafunzo kwa watoa huduma kutoka kote nchini Ethiopia ambao walitaka kujifunza jinsi ya kutengeneza na kutumia mbegu ya moja kwa moja inayovutwa na ng'ombe.

Baada ya kuandaa mafunzo, Alemo anashawishika kwamba anahitaji kununua kipanda kwa ajili ya shamba lake mwenyewe, na kama biashara ili kupata mapato kutokana na kupanda kwa wakulima wengine. tazama video hii kusikia mipango yake ya kupanua kilimo hifadhi kwenye shamba lake.

## Wasifu wa mshirika: Ofisi ya ODE (de Développement des Eglises Evangéliques)


Wanawake wakivuna mahindi ya kilimo hifadhi huko Koti

***Jean Twilingiyumukiza, Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha kati na Magharibi mwa Africa***

Office de Développement des Eglises Evangéliques (ODE) iliadhimisha miaka 50 ya huduma kwa Burkina Faso mwaka jana. ODE ni chama cha maendeleo kisicho cha faida kilichoundwa na Shirikisho la Makanisa ya Kiinjili na Misheni ya Burkina Faso (FEME) ili kukuza maendeleo endelevu, kuboresha utu wa binadamu na kujenga jamii yenye amani na haki zaidi. ODE inafanya kazi katika sekta za kilimo, rasilimali za maji (mabwawa, visima, na umwagiliaji), elimu isiyo rasmi na ujuzi wa kusoma na kuandika, na afya ya jamii.

Burkina Faso, "ardhi ya watu waaminifu," haina bandari katika Afrika Magharibi, na 86% ya wakazi wanategemea kilimo cha kujikimu. Nchi hiyo imekumbwa na ukame wa mara kwa mara na ukosefu wa usalama katika kipindi cha miaka 11 iliyopita. Kufikia mwishoni mwa 2021, ukosefu wa usalama nchini Burkina Faso ulisababisha watu milioni 1.4 kuyahama makazi yao na kusababisha uhaba mkubwa wa chakula na mahitaji mengine ya kibinadamu.



Miundo ya nusu mwezi hutumiwa kuvuna na kuhifadhia maji kwa ajili ya uzalishaji wa nafaka.

ODE ni mshirika wa muda mrefu wa Kamati Kuu ya Mennonite (MCC) Burkina Faso, na tangu 2013 imekuwa ikishirikiana na Benki ya Canadian Foodgrains kupitia MCC kuboresha usalama wa chakula kupitia uhamasishaji wa Kilimo Hifadhi (KH), uboreshaji wa uzalishaji wa mbegu, uzalishaji wa mboga mboga, elimu ya lishe. , na mafunzo ya viongozi wa jamii katika usimamizi endelevu wa ardhi vijijini.

Mradi wao wa sasa wa kilimo na maisha wa miaka mitano "PARSEO" unapanga kufikia kaya 1,130 (watu 6,780) katika vijiji 14 katika wilaya ya Oronkua. Kaya katika eneo hili hutegemea kilimo na mara nyingi hujitahidi kuzalisha chakula cha kutosha mwaka mzima na kupata mapato ya kutosha kukidhi mahitaji ya kimsingi. Upatikanaji wa maji ya kunywa na usafi wa mazingira pia ni mdogo. PARSEO itafanya kazi na jamii kushughulikia mahitaji haya kwa kukuza kilimo cha mashambani na upandaji bustani wa soko la umwagiliaji, kuanzisha vikundi vya kuweka akiba vya jamii, na kuwezesha upatikanaji wa maji ya kunywa, usafi na mifumo ya usafi wa mazingira.

Kama ilivyokuwa katika miradi ya awali (PROSAN-Yé na Koti), mradi wa sasa unakuza kilimo hifadhi pamoja na mazoea mengine ya kilimo, ikiwa ni pamoja na kujenga kwenye mabonde ya kiasi cha chini ya kulima yanayojulikana kama "zai" na "nusu-mwezi." Mazao ya kufunika mbolea ya kijani hukamilisha zai ya kitamaduni na hutoa kifuniko cha udongo na chakula cha mifugo. Kilimo hifadhi iliongeza kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa nafaka na mboga mboga na imeboresha lishe kwa zaidi ya washiriki 5,000 wa mradi katika vitongoji vya Yé na Koti. Washiriki wa mradi pia waliongeza uzalishaji wa kilimo bila msimu na umwagiliaji mdogo. PROSAN Koti alihimiza usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa wanawake 100 kutoka vijiji 11 kupitia uhamasishaji wa vikundi vya kuweka akiba vijijini.

# RATIBA ZA SAFARI ZA ALTA

## *Lilian Zheke*

**10-15 Julai, 2023**
***Zaka, Zimbabwe***
Mafunzo ya PAOZ

**14-24 Agosti, 2023**
***Kaskazini mwa Malawi***
Msaada wa mafunzo ya TSA na SOLDEV

**11-15 Septemba 2023**
***Mwandi,  Zambia***
Mafunzo na msaada wa UCZ

**25-29 Septemba 2023**
***Gutu & Zvishavane Zimbabwe***
*Ziara ya mafunzo na mabadilishano ZCC*

## *Jean Twilingiyumukiza:*

**9-15 Julai, 2023**
***Niamey, Niger***
Ziara ya mradi wa SPN na ujenzi wa timu

**24-28 Julai, 2023**
***Rubavu, Rwanda***
Mafunzo ya kufufua kwa wakufunzi wakuu

**5-11 Agosti, 2023**
***Bujumbura, Burundi***
Mafunzo ya uzamili ya kilimo hifadhi-kikao cha kwanza

**24-28 Agosti, 2023**
***Goma, DR Congo***
Warsha ya ngazi ya nchi

**10-15 Septemba, 2023**
***Bujumbura, Burundi***
Mafunzo ya uzamili ya kilimo hifadhi-kikao cha pili

## *John Kimathi Mbae*

**6  Julai, 2023**
***Nairobi, Kenya***
*Mahafali ya mkufunzi mkuu*

**10-15 Julai, 2023**
***Embu, Kenya***
Mafunzo ya ACC&S

**24-28 Julai, 2023**
***Kitui, Makueni, Machakos, Kenya***
Tembelea kubadilishana kwa Fadhili kwa KALRO na kituo cha kujumlisha

**1-4 Agosti, 2023**
***Tharaka Nithi, Kenya***
Kubadilishana mshirika  (Fadhili na NCCK)

**7-11 Agosti, 2023**
***Lodwar, Kenya***
Kutembelea ADRA

**21-25 Agosti, 2023**
***Marsabit, Kenya***
Mafunzo ya CITAM

**11-15 September, 2023**
***Tharaka, Kenya***
NCCK Training

**25-29 Septemba, 2023**
***Makueni, Kenya***
Mafunzo ya UDO

## *Neil Rowe Miller*

**17-19 Julai, 2023**
***Tarime, Tanzania***
*Mafunzo kwa watoa huduma*

**24-27 Julai, 2023**
***Bunda, Tanzania***
*Warsha ya nchi ya TZ*

**Agosti, 2023**
***Dodoma, Tanzania***
*Mafunzo kwa watoa huduma*

**Agosti, 2023**
***Kasulu, Tanzania***
*Kutembelea mradi wa CWS*